JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA

S. L.P 1055, ARUSHA
Simu : (027) 2503538/ 2507928
Nukushi: (027)
2505973
Barua
pepe:rbcarusha@pccb.go.tz
Wavuti : www.pccb.go.tz

ARUSHA-APRILI 21, 2021

TAARIFA KWA UMMA

TAKUKURU ARUSHA YAWAFIKISHA MAHAKAMANI WATUMISHI SITA (6) KWA MAKOSA YA RUSHWA NA UHUJUMU UCHUMI.

Ndugu Waandishi

Tumewaita hapa ili kupitia kwenu, tuendelee kuujulisha umma kwamba, kwa mujibu wa Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na. 11 ya mwaka 2007, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa mkoani Arusha,inaendelea na Uchunguzi wa Tuhuma mbalimbali na kwa mujibu wa chunguzi hizi kuwafikisha watuhumiwa mahakamani.

Ndugu Waandishi

Ofisi ya TAKUKURU Mkoani Arusha kwa kushirikiana na Ofisi ya Taifa ya Mashitaka imewafikisha mahakamani watuhumiwa wafuatao ;

- **Leonce Jacob Gully,**
- **Leah John Shashi na**
- **Ntimi Alijenti Mwakyembe**

Ambao wote ni wakazi wa Tarafa ya Eyasi iliyopo Halmashauri ya Wilaya ya Karatu ambao pia ni wafanyakazi wa mradi wa **Lake Eyasi Cultural Tourism Program** (LECTP) unaohusika kukusanya Ushuru wa utalii wa kitamaduni katika Kata ya Mang'ola Halmashauri ya Wilaya ya Karatu.

Washtakiwa hao wanatuhumiwa kuisababishia Halmashauri ya Wilaya ya Karatu hasara ya Jumla ya Shilingi Milioni Kumi na Moja, Laki Nne Elfu Tisa, na Arobaini na Tano (**Sh. 11,409,045/-)** katika kipindi cha Julai 2017 hadi Machi 2018 ambapo katika kipindi tajwa watuhumiwa wote watatu

walihusika kukusanya ushuru wa kiasi cha fedha cha **Sh. 11,409,045/-** lakini hawakukiwasilisha katika mamlaka husika ambayo ni Halmashauri ya Wilaya ya Karatu kama miongozo inavyowataka.

Watuhumiwa walifikishwa katika mahakama ya Hakimu Mfawidhi wa Wilaya ya Karatu mnamo tarehe 20.04.2021 kwa makosa ya Uhujumu uchumi ambayo ni ufujaji wa fedha za Umma kinyume na Kifungu cha 28(1) cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, [CAP 329 R.E 2019] pamoja na kosa la Kuisababishia Serikali hasara kinyume na Aya ya 10 (1) ya Jedwali la kwanza ikisomwa pamoja na vifungu vya 57 (1) na 62 (2) vya Sheria ya Uhujumu Uchumi [CAP 200 R.E 2019] makosa ambayo/vitendo ambavyo vilipelekea Halmashauri ya Wilaya ya Karatu kupata Hasara ya fedha tajwa. Washitakiwa walifunguliwa shauri ambalo ni **ECC. Na. 02/2021.**

Katika tukio la pili, ofisi ya TAKUKURU Mkoani Arusha imewafikisha mahakamani watuhumiwa wafuatao ;

- **Cleophas Anton Tenganamba**,
- **Josephine Innocent Msuya** na
- **Rose Lorivi Kipuyo**

Ambapo **Cleophas Anton Tenganamba** na **Josephine Innocent Msuya** walikuwa ni watumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Longido katika kitengo cha manunuzi na wamefikishwa katika mahakama ya Hakimu Mfawidhi wa Wilaya ya Longido mnamo tarehe 20.04.2021 kwa kosa la kutumia nyaraka za uongo [uttering false document] kinyume na Kifungu cha 342 cha Sheria ya Kanuni za Adhabu, [CAP 16 R.E 2002] ambapo walifunguliwa Shauri la Jinai **Na. 49/2021**. Watuhumiwa walipaswa kufanya manunuzi ya mifuko ya Saruji 2,400 kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha afya Engarenaibor, ila mifuko ya saruji 180 haikuwasilishwa, hata hivyo katika taarifa yao waliandika uongo wakionyesha wamewasilisha mifuko yote wakati sio kweli.

Aidha katika shauri lingine mtuhumiwa **Rose Lorivi Kipuyo** aliyekuwa Afisa Mtendaji wa Kijiji cha Oltepesi katika Halmashauri ya Wilaya ya Longido alifikishwa mahakamani mnamo tarehe 20.04.2021 kwa kosa la

kutumia nyaraka za uongo [uttering false document] kinyume na Kifungu cha 342 cha Sheria ya Kanuni za Adhabu, CAP 16 R.E 2019] ambapo alifunguliwa Shauri la Jinai Namba **51/2021.** Mtuhumiwa aliandika barua kuonyesha kuwa Serikali ya Kijiji tajwa iligawa viwanja kwa wananchi, taarifa ambayo haikuwa sahihi.

Wakati huo huo, Ofisi ya TAKUKURU Mkoani Arusha mnamo tarehe 20.04.2021 ilishinda Shauri namba **CC. Na. 193/2020** lililokuwa likiendelea katika Mahakama ya Wilaya ya Arusha dhidi ya **Elias Samwel Mollel** aliyekuwa akituhumiwa kujihusisha na vitendo vya rushwa kwa kumuhonga askari polisi ili ampatie dhamana ndugu yake aliyekuwa anashikiliwa katika kituo cha polisi, kosa ambalo ni kinyume na kifungu cha 15 (1) (b) cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, [CAP 329 R.E 2019]. Mshitakiwa huyo alikutwa na hatia na kuhukumiwa adhabu ya kulipa faini ya **Tshs. 500,000/-** au kwenda jela **miaka mitatu. Mtuhumiwa amelipa Faini.**

Katika tukio jingine ofisi ya TAKUKURU Mkoa wa Arusha imefanikiwa kuokoa kiasi cha shilingi Milioni Kumi Laki Tatu na Elfu Themanini **(Sh. 10,380,000/=)** zilizokuwa zimechepushwa na kufanyiwa ubadhilifu kinyume na Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na. 11 ya Mwaka 2007, fedha ambazo ni stahiki za waliokuwa watumishi wa **World Vision** Mkoa wa Arusha.

Watumishi hao ni **Bw. Eliahu Luka Laizer** na Bi. **Sarah Samwel Msuya** ambao walipata ajali wakiwa kazini mnamo mwaka 2009 lakini hawakuwa wamelipwa fedha zao kama ambavyo sheria ya fidia kwa wafanyakazi inavyoelekeza (**Workers Compesation Fund-WCF**) mpaka TAKUKURU Mkoa wa Arusha ilivyoingilia kati mnamo Februari, 2021.

TAKUKURU Mkoani Arusha inawaasa watumishi na wananchi wote wa mkoa wa Arusha, kuepuka kujihusisha na vitendo vya rushwa, ambavyo vitasababisha kuchukuliwa hatua kali za kisheria.

Imetolewa na:

JAMES G.RUGE
MKUU WA TAKUKURU (M)
ARUSHA.